

**HOTUBA YA MHESHIMIWA MKUU WA
MKOA WA RUKWA ZELOTE STEPHEN
ZELOTE KATIKA UFUNGUZI WA MAFUNZO
YA WAMILIKI NA WAFANYABIASHARA WA
PEMBEJEO (MBOLEA, MBEGU NA
VIUATILIFU) ZA KILIMO KATIKA MKOA WA
RUKWA TAREHE 27 APRILI, 2017**

*Ndugu wawezeshaji wa mafunzo (Wizara ya
Kilimo – Kitengo cha Mbegu,*

*Mamlaka ya Mbolea TPRI, Taasisi ya madawa
TPRI na Baraza la utunzaji wa Mazingira NEMC
Kanda ya Mbeya,*

*Ndugu wamiliki na wafanyabiashara ya pembejeo
za Kilimo,*

Ndugu wakulima wakubwa,

*Ndugu Maafisa Ugani kutoka Halmashauri za
Mkoa wa Rukwa,*

*Mfadhili wa mafunzo (Shirika la Maendeleo la
Uholanzi (SNV),*

*Wawakilishi kutoka makampuni mbalimbali ya
Mbolea, Mbegu na Viuatilifu,*

Wataalam wa Kilimo kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa,

Waandishi wa habari,

Mabibi na Mabwana.

Nawashukuru kwa kunipa heshima ya kufungua mafunzo yenu ya Wamiliki na wafayabiashara wa Pembejeo za Kilimo ikiwa ni Mbolea, Mbegu na Viuatilifu ambayo imeandaliwa na Shirika la Maendeleo la Uholanzi kituo cha Rukwa leo tarehe 27 Aprili, 2017 katika ukumbi huu.

Ndugu Wawezeshaji,

Nichukue nafasi hii kuwapongeza Shirika la Maendeleo la Uholanzi kwa kukubali kuwezesha mafunzo haya kufanyika katika Mkoa wetu ambao ni maarufu kwa shughuli za Kilimo cha mazao ya chakula. Lakini ni vema niwashukuru wale wote ambao wamejiandaa kutoa mafunzo kwa walengwa ambao ni wakulima na wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo. Ni vema niwataje kwamba ni wale kutoka Kitengo cha

Mbegu, Taasisi ya Madawa (TPRI) na Baraza la Utunzaji wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Mbeya.

Ndugu Wawezeshaji,

Nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Wafanyabiashara wa Pembejeo za Kilimo ambao wamekuwa wakitimiza huduma hiyo kwa uadilifu, umakini kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu kuhakikisha kwamba Wateja wao ambao ni Wakulima wanapata Pembejeo zilizokuwa sahihi tofauti na baadhi ambao wamekuwa wakiwahudumia wakulima kwa kuwauzia Pembejeo ambazo sio halisi au zilizochakachuliwa. Sote tunajua madhara ambayo yamekuwa yakiwakabili wakulima kwa kutopata Pembejeo halisi. Serikali ya Mkoa kwa kupitia kamati za usambazaji Pembejeo imekuwa ikikemea na kuchukua hatua kadhaa kuona kwamba inawalinda wakulima kuingizwa katika janga la Pembejeo feki. Hatua mnayoichukua ya kutoa mafunzo ya siku 3 ni jambo la msingi sana naamini kupitia mafunzo haya itawarejesha wale wote ambao wanatumia ujanja kuharibu utaratibu

mzuri unaosimamia kuwapatia wakulima Pembejeo sahihi watajirekebisha.

Ni matumaini yangu vilevile kwamba Mamlaka zinazohusika kusimamia eneo hili muhimu la Pembejeo kwa maana ya Mbegu, Mbolea na Viuatilifu watapata nafasi ya kuona na kuelewa changamoto zilizopo kwa wasambazaji wa pembejeo zinazohusika.

Ndugu Wawezeshaji,

Nataka niwakumbushe wote kwa pamoja kwamba Serikali ya Awamu ya 5 imepania kuwa na viwanda katika maeneo mbalimbali ya Nchi ikiwemo Mkoa wa Rukwa. Watumiaji wa Pembejeo mnapotimiza wajibu wenu kwa usahihi maana yake ni kwamba wakulima watazalisha chakula cha kutosha na viwanda vyote vitakavyokuwepo vitapata malighafi vitakavyotumia kwenye viwanda kwa lengo la kuinua thamani ya mazao ya wakulima na kuwaletea manufaa ya kutosha.

Ndugu Wawezeshaji,

Hivyo nataka kuisitiza kwamba kuanzia sasa Mamlaka zinazohusika kusimamia Taratibu Kanuni na Sheria za Pembejeo zijihimu katika kusimamia ubora na usambazaji wa pembejeo zote. Ni wakati muafaka sasa taasisi zote zinazohusika na tafiti za Mbegu na uzalishaji wake ziendeleo na juhudi za kuona kwamba uzalishaji wa Mbegu zinazostahili kwa mazingira yetu inaongezeka kuliko kutegemea za kutoka sehemu zingine ambazo hatuna uhakika na usalama wake.

Ndugu Wawezeshaji,

Mwisho ni matumaini yangu kwamba mafunzio haya hayataishia kuwa ndani ya ukumbi huu bali yatatolewa nje kupata utekelezaji kwa vitendo. Ni vizuri mkafahamu kwamba malalamiko ya wakulima yapo mengi katika eneo hili la pembejeo jambo ambalo mnapaswa kulijua na kuchukua hatua zinazostahili ili kuwajengea uhalali wa wajibu wenu na biashara mnayofanya. Taratibu ya ninyi kuwa wafanyabiashara wa Pembejeo

mtazifahamu na mamlaka zinazohusika ikiwepo; Mamlaka ya uthibiti ubora wa Mbolea Tanzania (TFRA), Taasisi ya kudhibiti ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) na Taasisi ya utafiti wa viuatilifu vya Kilimo Tanzania (TPRI).

Nitumie nafasi hii kuagiza Halmashauri zote kuhakikisha kwamba wanasimamia kikamilifu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazotawala Pembejeo za aina zote; na vyombo vya Sheria vihakikishe kwamba wale wote wanaofikishwa mbele yao kwa kukiuka Taratibu, Kanuni na Sheria wanashughulikiwa kikamilifu bila huruma.

Nawatakia kila la heri katika mafunzo haya.

Zelote Stephen Zelote

MKUU WA MKOA WA RUKWA